

TOLEO LA. 08


Jarida la *Ni Magufuli Tena*

2020 - 2025

ALIAHIDI | AMETEKELEZA | APEWE TENA 5 | 7 SEPTEMBER, 2020



MAGUFULI AVUNJA REKODI KIRUMBA



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**



RAIS MAGUFULI AANIKA MAFANIKIO JIJINI MWANZA

- Kulifanya Jiji la Mwanza Kitovu cha Biahara Afrika Mashariki

Na Mwandishi Wetu - **MWANZA**

Mgombea Urais wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli ameanika mafanikio makubwa ya Serikali katika kipindi cha miaka mitno na kuahidi kuendeleza jitihada za kulifanya Jiji la Mwanza kuwa Kitovu cha Biashara katika ukanda wa Maziwa Makuu.

“Kwa usafiri wa majini, tumejenga chelezo ya kujengea na kukarabati meli, tumefanya ukarabati wa meli tano, tumejenga meli mpya kwa shilingi bilioni 152, tumejenga vivuko vya MV Mwanza na Mv Ilemela kwa gharama ya shilingi bilioni 2.7 na cha tatu kinaendelea kujengwa kwa shilingi bilioni 4.2,” ameeleza Rais Magufuli leo jijini Mwanza katika mkutano wa kampeni ulifanyika katika Uwanja wa CCM Kirumba na kuhudhuriwa na maelfu ya wananchi wa jiji hilo.

Amesema katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/21 shilingi bilioni 15 zimetengwa kwa ajili ya kufanya ukarabati mkubwa wa meli zingine ikiwemo MV Umoja ili iweze kubeba mabehewa mengi zaidi kwenda nchi jirani. “Wafanyabiashara wanaotumia

usafiri wa majini wanafahamu tani moja ya mzigo kutoka Bukoba ilikuwa ikibebwa kwa shilingi 130,000 kwa kutumia barabara lakini leo kwa meli tani moja inabebwa kwa shilingi 27,000”, alibainisha Rais Dkt. Magufuli na kuongeza kuwa mpango wa baadae ni kujenga meli kubwa ya mizigo itakayofanya safari kwenda Uganda, Kisumu-Kenya, Musoma na Mwanza.

Kwa upande wa upanuzi wa uwanja wa ndege wa Mwanza, amesema kuwa kazi iliyofanyika ni kurefusha njia yake kutoka Kilometa 2.8 hadi Kilometa 3.5 na kuwezesha kubwa za abiria na mizigo kutua kwenye uwanja huo na zinakwenda moja kwa moja Ulaya. “Tangu Aprili mwaka huu mpaka sasa tumesafirisha tani 109,503 za mabondo ya samaki kupitia uwanja huu wa Mwanza. Anayesema ndege hazina faida aje awaulize wavuvi wa mkoani hapa,” amesisitiza Rais Magufuli.

Huduma za afya zimeboreshwa ambapo Rais Magufuli amesema kuwa huduma za kibingwa zinatolewa katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Bugando ambapo kwa sasa wagonjwa wa moyo, wagonjwa wa kansa na wagonjwa mahututi watahudumiwa hapo na kwamba Serikali imepeleka vifaa vya kisasa ikiwemo CT SCAN 128, Utra sound 12, Digital X- ray, radiotherapy na kujenga miundombinu mingine kwa gharama ya shilingi bilioni 11.4.

Ameongeza kuwa upanuzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Sekou Toure unaendelea na utagharimu shilingi bilioni 11.1 ikiwemo kujenga wodi ya wakina mama na watoto. “Tumejenga na kufanya upanuzi wa hospitali za wilaya sita pamoja na ujenzi wa vituo vya afya 14 kwa jumla ya shilingi bilioni 13, wataalam wa afya wapatao 147 waliajiriwa katika mkoa wa Mwanza na kuongeza bajeti ya dawa kutoka shilingi bilioni 2.44 mwaka 2015 hadi bilioni 9.07 mwaka 2020, na tumeleta magari 11 na boti moja kwa ajili ya kubebea wagonjwa,” ameleza Rais Magufuli.

Aidha, katika sekta ya elimu, Rais Dkt. Magufuli amesema kuwa Serikali imeongeza nyumba, madarasa, maabara pamoja na mabweni, kukarabati shule sita kongwe pamoja, chuo cha ualimu kimoja na kutoa elimu bila malipo kwa gharama ya shilingi bilioni 53.7 katika mkoa wa Mwanza. Katika miundombinu, Rais amesema Serikali imekamilisha ujenzi wa barabara ya Usagara - Kisesa kwa kiwango cha lami yenye urefu wa Kilometa 17 kwa gharama ya shilingi bilioni 20.1 na kuzitaja barabara zingine kuwa ni Mwanza-Airport, Nyakato-Buswelu, Makongoro-Mwaloni, Isamilo-Mjimwema, Pasiansi-Buzuruga pamoja, daraja la Furahisha pamoja na kuanza ujenzi wa Stendi Kuu ya Nyegezi na daraja la Kigon-go-Busisi ambalo ni moja kati ya madaraja marefu zaidi Afrika Mashariki lenye jumla ya Kilometa 3.2 kwa gharama ya shilingi bilioni 300.

“Tumeanzisha soko la kimataifa la madini hapa Mwanza na tangu lianzishwe mwezi Mei, 2019 zaidi ya kilo 2,252.2 za dhahabu zimeuzwa kwa shilingi bilioni 228.37 ambapo kati ya mauzo hayo, kilo 1,652.68 zenye thamani ya shilingi bilioni 166.87 zimetoka nje ya mkoa wa Mwanza. Bapa Mwanza tumetoa leseni 147 kwa wachimbaji wadogo na tumeanza ujenzi wa kiwanda kikubwa cha kusafisha madini kitakachokuwa na uwezo wa kusafisha kilo 500 za dhahabu kwa siku”, alieleza Rais Magufuli na kuomba wananchi kumchagua ili afanye mabadiliko makubwa zaidi yenye kuwanufaisha.



MAGUFULI AZIDI KUPATA BARAKA ZA VIONGOZI WA DINI

Na Mwandishi Wetu - **MWANZA**

Viongozi wa Dini mkoa wa Mwanza wamemng'arisha kwa dua na sala Mgombea Urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli ili Mungu amlinde na kumsimamia katika kampeni zake ilia pate kibali cha kuwatumia tena watanzania kwa kipindi cha miaka mitano.

"Tumeshuhudia Kiongozi wetu John Pombe Magufuli akipiga vita rushwa, ufisadi na akimtanguliza Mwenyezi Mungu," inaeleza sehemu ya maombi ya Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Sheikh Hassan Kabeke wakati wa dua akiombea kampeni za mgombea huyo wakati wa mkutano wa kuomba kura uliofanyika uwanja wa CCM Kirumba Jijini Mwanza.

Katika maombi hayo, Sheikh Kabeke aliendelea kumwombea Rais Magufuli akisema: "Umlinde na kumhifadhi Rais wetu. Waislamu wa Mwanza na watanzania hatuna cha kumlipa bali kukuomba Mwenyezi Mungu umlinde na umsaidie katika nia yake ya kuendelea kuwaongoza watanzania.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa Askofu Mkuu wa Jimbo Katoliki la Mwanza, Padri Joseph Mchole alisema: “Tunamuomba katika kampeni na umkinge mgombea huyu na kila adui, uilinde nchi yetu na kuwaangazia viongozi wetu”, alisikiaka Padri Mchole katika sehemu ya maombi yake.

Alimuomba Mwenyezi Mungu ailinde Tanzania na kuwaangalia viongozi wake kuwa na moyo wa kujitolea kufanya kazi kwa ajili ya kuwaletea maendeleo.

Kwa upande wake, Askofu wa Kanisala Africa Inland Church (AIC), Philip Mafuja aliomba Mungu aipe Tanzania kiongozi mchapakazi na Mchamungu atakaye imarisha umoja na mshikamano kwa watanzania.

Mwaka 2015 Viongozi wa Dini pamoja na watanzania walimuomba Mwenyezi Mungu awapatie kiongozi atakayeenzi amani, umoja, upendo, mshikamano na atakayewatumikia watanzania kwa moyo mmoja. Katika Uchaguzi huo Rais Magufla alishinda na katika kipindi cha miaka mitano amefanya mabadiliko makubwa ambayo yamewanufaisha watanzania wote wakiwemo wale wa hali ya chini.



RAIS MAGUFULI APIGA SIMU ROMBO, AOMBA WANANCHI WAMCHAGUE PROFESA MKENDA

Na Mwandishi Wetu - **Rombo - KILIMANJARO**



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Mgombea wa nafasi ya Urais kupitia CCM, Rais Dkt. John Pombe Magufuli amewaomba wakazi wa Tarakea wamchague Profesa. Adolf Mkenda kwa kuwa anauwezo mkubwa wa kuwatumikia na kuwaletea maendeleo.

Ameyasema hayo leo Septemba 7, 2020 alipozungumza na wakazi wa Tarakea kupitia simu aliyompigia Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ambaye alikuwa akihutubia mkutano wa kampeni uliofanyika kwenye uwanja wa Polisi Tarakea, wilaya Rombo, Mkoani Kilimanjaro.

“Watu wa Tarakea nawaomba mumchague Profesa Mkenda msifanye makosa tena. Profesa Mkenda alikuwa Katibu Mkuu wangu na amefanyakazi nzuri na nilimruhusu kuja kugombea ubunge katika jimbo la Rombo. Rombo nawaomba mnipigie kura, tunataka tulete mabadiliko makubwa nchini,” aliongea Rais Magufuli.

Kwa upande wao, wakazi wa Rombo amesema wamefurahishwa sana na heshima kubwa waliyopewa na Rais Dkt. Magufuli hivyo watahakikisha siku ya kupiga kura watamchagua Magufuli pamoja na mgombea ubunge Profesa Mkenda na wagombea udiwani wote kwa tiketi ya CCM.



UHUSSIANO WA KIMATAIFA UMEIMARIKA ZAIDI KATIKA AWAMU YA TANO

Na Mwandishi Wetu

Katika kipindi cha miaka mitano ya Serikali ya Awamu ya Tano, Uhusiano wa Tanzania na nchi zingine duniani pamoja na mashirika ya kimataifa umekua na kuimarika zaidi na kuwezesha Tanzania kufungua balozi nyingi nje ya nchi na mataifa ya nje kufungua balozi zao hapa nchi.

Mgombea Urais kwa tiketi ya Chama cha Mapindizi (CCM), Rais Dkt. John Pombe Magufuli ameeleza leo jijini Mwanza ambapo amesema katika miaka mitano Tanzania imefungua balozi katika nchi za Algeria, Cuba, Israel, Korea Kusini, Qatar, Namibia, Sudan na Uturuki, na kwamba Tanzania itaendelea kuteua mabalozi katika nchi mbalimbali. Aidha, nchi za Ethiopia na Poland zimefungua balozi zao hapa nchini na hakuna nchi ambayo imevunja uhusiano wake na Tanzania.

"Sina uhakika kama kuna wakati tuliwahi kufungua balozi nyingi kama kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Tano, tumeaminiwa sana hata kupewa Uenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) pamoja na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)", alisema Rais Magufuli.

Mbali na kufungua balozi, nchi ya Tanzania imetembelewa na viongozi wa nchi na Taasisi mbalimbali za kimataifa zikiwemo za Vietnam, India, Uturuki, Afrika Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Ethiopia, Misri, Rwanda, Zambia, Zimbabwe, Uganda, Shirika la Fedha Duniani (IMF), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) pamoja na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD).

Kuongezeka kwa ofisi za ubalozi wa Tanzania katika mataifa mengine na mataifa ya nje kufungua balozi zao hapa nchi ni kielelezo tosha cha jinsi uhusiano mzuri wa kidiplomasia kati ya Tanzania na mataifa mbalimbali duniani na kufuta kabisa uzushi, uzandiki na upotoshaji wa baadhi ya wanasiasa kwamba Tanzania haina uhusiano mzuri na mataifa mengine.



MAJALIWA: SERIKALI INA FEDHA ZA KUTOSHA KUWAHUDUMIA WATANZANIA

Na Mwandishi Wetu - **Rombo** - **KILIMANJARO**

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa amesema Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli ina fedha za kutosha kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania katika kuboresha huduma za jamii zikiwemo za afya, maji, elimu.

Mhe. Majaliwa amsema hayo leo Jumatatu, Septemba 7, 2020 alipohutubia mkutano wa kampeni uliofanika katika uwanja wa soko la Holili wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro ambapo amemuomba kura Rais Dkt. Magufuli na mgombea ubunge wa Jimbo la Rombo Profesa Adolf Mkenda na wagombea udiwani kupitia CCM.

Mheshimiwa Majaliwa amewataka wananchi wasifanye mzaha siku ya kupiga kura itakapofika, wasimchague mtu kwa sababu ya ushabiki na badala yake wamchague Rais Dkt. Magufuli na wagombea wote wa CCM ili waweze kushirikiana nao katika kuendeleza miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao.

“Tunaomba kura zenu Wana-Holili na watanzania wote kwa Rais Dkt. Magufuli ili akaendeleo kuboresha maendeleo katika sekta ya elimu itakayotuwzesha kuwa na wataalamu wengi. Nawaomba mumchague Dkt. Magufuli kwa sababu ameitendea haki nchi yetu na ni kiongozi mcha Mungu na mpenda maendeleo.”

Akizungumzia kuhusu changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama inayowakabili wakazi wa Holili, Mhe. Majaliwa amesema tayari Serikali imetoa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kufanya utafiti wa kina kuona namna watakavyoyatoa maji kutoka Ziwa Chala na kuyasambaza kwa wananchi.

Ametaja mradi mwingine wa maji unaotekelezwa katika wilaya hiyo ni mradi wa maji Njoro II uliopo Tarake). "Serikali imekamilisha mradi huu kwa shilingi milioni 200 na unatoa huduma ya maji katika eneo la Tarakea. Malengo ya Serikali kwa sasa ni kutafuta fedha ili kuupanua mradi huo uweze kutoa maji katika maeneo mengine ya Tarafa

nzima ya Tarekea," alieleza Mhe. Majaliwa.

Amesema mradi wa kijiji cha Ngareni wenye thamani ya shilingi milioni 812.4 uliohusisha ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji la lita 75,000 na ujenzi wa vituo 15 vya kuchota maji pamoja na ufungaji wa bomba za njia kuu na njia za kusambaza maji umekamilika.

Amesema kuwa katika kuhakikisha huduma ya maji na salama inawafikia wakazi wote wa wilaya ya Rombo kika-milifu, Serikali mwezi Julai mwaka huu imevunja Kampuni ya Maji ya Kill Water na kuanzisha Mamlaka ya Maji (ROWA-SA).





KALI ZA MAGUFULI MWANZA SEPTEMBER 7, 2020

- 1.** TUMEFANYA UPANUZI WA UWANJA WA NDEGE WA MWANZA KWA KUREFUSHA NJIA YAKE KUTOKA KM 2.8 HADI KM 3.5, TUMEWEKA TAA NA JENGO LA KUONGOZEA NDEGE NA ENEO LA KUEGESHEA NDEGE ZA MIZIGO, TUMEJENGA RADA KUBWA, TUMEWEKA MIUNDOMBINU YA KUHI-FADHI MINOFU NA UJENZI WA JENGO LA ABIRIA UNAENDELEA.
- 2.** KATIKA MIAKA MITANO ILIYOPITA TUMEFUNGUA BALOZI MPYA 8 NA NCHI MBILI ZIMEFUNGUWA BALOZI ZAO HAPA TANZANIA, HAKUNA NCHI YOYOTE AMBAYO IMEVUNJA UHUSIANO NA NCHI YA TANZANIA.
- 3.** DARAJA LA KIGONGO-BUSISI AMBALO NI MIONGONI MWA MADRARAJA MAREFU AFRIKA MASHARIKI LENYE UREFU WA KM 3.2 LIMEANZA KUJENGWA KWA GHARAMA YA SHILINGI BILIONI 300.
- 4.** KATIKA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2020/21, TUMETENGA SHILINGI BIL.15 KWA AJILI YA KUFANYA UKARABATI MKUBWA WA MELI ZINGINE IKIWEMO MELI YA MV UMOJA ILI IWEZE KUBEBA MABEHWA MENGI ZAIDI.
- 5.** "NDUGU ZANGU WANGAPI MNAOSEMA MTANIPA KURA??? SEMENI NDIO ILI WANAFIKI WAIPATEPATE"



TUCHAGUE VITENDO SI MANENO - SHIGONGO

Na Mwandishi Wetu - **MWANZA**

Mgombe Ubunge Jimbo la Buchosa, Eric Shigongo amewaomba wataanzania kuchagua kiongozi anayefanya kazi na kutekeleza ahadi kwa vitendo ili kuleta maendeleo badala ya wagombea ambao wanatoa ahadi wakati hata hawajawahi kutekeleza kufanya jambo linaloonrkana.

Amesema kuwa Rais Magufuli ametekelea ahadikwa vitendo hivyo wananchi hawana budi kumchgua tena na kuachana na wapinzani ambao wanataka kufanya majaribio ya kuongoza nchi wakati hawana hata jambo moja walilowahi kutekeleza.

kwa vitendo na si maneno Ili kuifanya Tanzania iendele kupiga hatua zaidi kimaendeleo inahitaji viongozi Tanzania inapaswa kuchagua viongozi walion

esha uwezo wa kufanya kazi na wenye kuongea maneno matupu ambayo hayatawasaidia Watanzania.

“Hakuna kitu kibaya kama kufanya majaribio kwenye uongozi, tuchague yule aliyeonesha kuwatumikia wanachi kwa dhati na si mwingine ni John Pombe Magufuli,” alisisitiza Shigongo na pia kuwaomba kura wananchi wa wa Buchosa kumchgua awe Mbunge wao.

Kwa upande wake, Alexander Mnyeti amewaomba wananchi wa Mwanza kuvunja rekodi ya miaka yote. “Tunataka tushindane katika majimbo ya kupata kura nyingi za magufuli ili wapinzani wajue hii kazi ya Urais sio ya kuwapa watu ambao hawana uchungu na nchi,” alisisitiza Mnyeti ambaye katika jimbo lake amepita bila kupingwa.

Jarida la Ni Magufuli Tena

2020 - 2025



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**